# Non-Technical Summary

**1. Utangulizi wa Mradi**

Kampuni ya Guangzhou Iceberg Environmental Consulting Services Co., Ltd. (hapa inajulikana kama Iceberg), kampuni ya Kichina inayojitolea kuokoa nishati na kupunguza umaskini kwa nchi zinazoendelea kupitia fedha za kaboni, itashirikiana na washirika wa ndani kutekeleza mradi wa majiko banifu nchini Tanzania.

Mradi huu hautatoa tu majiko yanayookoa nishati na pesa kwa jamii za hapa, bali pia utatoa fursa za ajira kwa jamii wakati wa utekelezaji wake na kuboresha viwango vya maisha kwa watu wa vijijini ambao ndio watumiaji wakuu wa majiko hayo.

Mradi huu utaomba kusajiliwa kama mradi wa kupunguza hewa ukaa chini ya kiwango cha kimataifa kinachoitwa “Gold Standard for Global Goals”. Iceberg itamiliki kikamilifu hati zote za kaboni zitakazozalishwa na mradi huu. Mapato yatokanayo na mauzo ya hati hizo katika soko la kimataifa la kaboni yatathibitisha uendelevu na upanuzi wa mradi.

Majiko banifu yaliyopangwa kusambazwa yanaonyeshwa hapa chini



Muda wa mradi unatarajiwa kuwa miaka kumi. Kiwango cha mradi kitaamuliwa baada ya mashauriano na wadau wa ndani.

**2. Mpango wa Utekelezaji**

Iceberg inapanga kushirikiana na washirika wa ndani kusambaza majiko banifu katika maeneo ya vijijini nchini Tanzania. Mpango wa utekelezaji ni kama ifuatavyo:

Tathmini ya Mahitaji: Kufanya tathmini kubaini maeneo ambayo usambazaji wa majiko banifu utakuwa na manufaa zaidi. Kutambua kaya zinazotegemea majiko ya kienyeji na ambazo zina uhitaji mkubwa zaidi.

**Ushirikiano:** Kushirikiana na washirika wa ndani kuhakikisha majiko banifu yanafika katika jamii

lengwa. Hii itasaidia Iceberg kupata upatikanaji wa jamii, kutambua wasambazaji wa ndani, na kupata vibali na ruhusa kutoka serikalini. Kaya ambazo tayari zimeshiriki kwenye miradi kama hii hazitajumuishwa.

**Ununuzi:** Kutambua wasambazaji bora na wa gharama nafuu wa majiko banifu. Kuhakikisha majiko hayo yanakidhi viwango vya ubora na usalama.
**Usambazaji:** Washirika wa ndani watasimamia usambazaji. Wataandaa mpango wa usafirishaji wa majiko hadi jamii husika. Pia watahakikisha majiko yanafika kwa kaya zinazoyahitaji zaidi kwa ufanisi na kwa gharama nafuu.

**Mafunzo**: Kuwapa washirika wa ndani mafunzo ya kutosha ili waweze kutekeleza mradi kwa urahisi. Baadaye wao watawafundisha wanufaika kutu inmia majiko kwa usalama na ufanisi, pamoja na namna ya kuyatunza.

**Ufuatiliaji na Tathmini:** Kuandaa mpango wa kufuatilia maendeleo ya usambazaji na matumizi ya majiko pamoja na athari zake kwa jamii. Mfumo wa maoni kutoka kwa wanufaika pia utaanzishwa.

**Uendelevu:** Kuandaa mpango wa kuhakikisha mradi unadumu kwa muda mrefu, ikiwemo mafunzo kwa mafundi wa ndani kukusanya mrejesho na kutunza majiko.

**Mawasiliano na Uhamasishaji:** Kuandaa mpango wa mawasiliano na uhamasishaji kuhusu manufaa ya majiko banifu na maendeleo ya mradi kupitia vyombo vya habari, ushirikishwaji wa jamii, na mitandao ya kijamii.

### 3. Athari za Kiuchumi, Kijamii na Kimazingira za Mradi
#### 3.1 Athari za Kiuchumi
Mradi utapunguza gharama za ununuzi wa kuni kwa kaya.
Mradi utasaidia kukuza biashara na mashirika ya ndani, na kuunda ajira kupitia utengenezaji, usafirishaji na usambazaji wa majiko.

#### 3.2 Athari za Kijamii
Mradi utapunguza matumizi ya fedha kwa kuni kutokana na ufanisi wa juu wa joto.
Utapunguza mzigo wa kukusanya kuni, hasa kwa wanawake na wasichana.
Utaboresha viwango vya maisha vya wananchi wa Tanzania.

#### 3.3 Athari za Kimazingira
Mradi utapunguza gesi chafuzi zitokanazo na uchomaji wa kuni.
Njia ya jadi (mawe matatu) huzalisha moshi hatari kwa kiwango kikubwa; mradi utapunguza uchafuzi wa hewa majumbani.
Mradi utapunguza mahitaji ya kuni, hivyo kulinda misitu na kuendeleza bayoanuwai.

## 4. Muhatasari wa mchango unaotarajiwa wa mradi kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

| **Malengo ya maendeleo Endelevu yanyolengwa** | **Kiashiria cha SDG** | **Athari** |
|---|---|---|
| Lengo1: kutokomeza umaskini | 1.1.1:Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umasikini wa kimataifa kwa jinsia, umri, hali ya ajira na eneo(mjini/vijijini} | Jiko bora ni huduma ya msingi inayohitajikaili kuishi Maisha yenye afya na tija, ikiwemo kuokoa mud ana pesa za kuni katika kaya |
| Lengo2: kutokomeza Njaa | 2.1.1 Kiwango cha upungufu wa lishe | Mradi utaboresha usalama Wa chakula na hali ya lishe,hasa kwa Watoto na wanawake, kwa kupunguza kupika kusikotosha, mzigo wa kukusanya kuni, muda wa kuandaa chakula na gharama za kuni |
| Lengo 3:Afya Bora na Ustawi | 3.2.1 Kiwango cha vifo vya Watoto chini ya miaka mitano | Kwa kutumia ICS, watu watapunguza kuathirika na chembechembe ndogo hatari na gesi ya CO kutokana na ufanisi mkubwa wa mwako, unaosababisha upikajia haraka na mwako kamili Zaidi.Pia itapunguza hatari ya kuungua,hasa kwa Watoto wadogo |
| Lengo 4: Elimu Bora | 4.3.1 Asilimia ya vijana na watu wazima waliopata elimu na isiyo rasmi katika kipindi cha miezi 12 iiyopita,kwa jinsia | Mradi utatoa elimu na mafunzo yasiyo rasmi kwa watumiaji kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi, maendeleo endelevu, n.k |
| Goal 5: Usawa wa kijinsia | 5.4.1 Uwiano wa muda unaotumika kwenye kazi za nyumbani na malezi zisizolipwa, kwa jinsia, umri na eneo | Mradi utapunguza kazingumu kwa wanawake na Watoto kwa kuokoa muda wa kukata,kukusanya na kubeba kuni Pamoja na kuni Pamoja na kupika kwa moto na wazi wenye moshi |

| | | |
|---|---|---|
| Lengo 7: Nishati safi na salama | 7.1.2 Asilimia ya wat wanaotumia nishati safi na teknolojia kama chanzo kikuu cha nishati | Majiko bora yaliyosambazwa na teknolijia safi ya kupikia. Mradi utaongeza idadi ya watu wanaotumia nishati safi na teknolojia |
| Lengo 8:Kazi Bora na ukuaji wa uchumi | 8.3.1Uwino wa ajira zisizo rasmi kati ya ajira zote, kwa sekta na jinsia.<br>8.5.1 Mapato ya wafanyakazi wa kike na kiume, kwa kwzi, umri na watu wenye ulemavu | Mradi utatoa nafasi za ajira kwa watu wa ndani bila kujali jinsia au umri |
| Lengo 9: Viwanda, ubunifu na Miundombinu | 9.3.1 Uwiano wa viwanda vidogo katika mchango wa jumla wa viwanda | Viwanda vya ndani vinavyotengeneza majiko bora ni viwanda vidogo.Vitapanua uzalishaji ili kukidhi mahitaji, na ,mlolongo mzima wa usambazai utanufaika |
| Lengo 13: Hatua dhidi ya tabianchi | 13.0.Kiasi cha tani za gesi chafuzi zilizozuiliwa au kupunguzwa | Mradi utapunguza gesichafuzi kutokana na kuchoma kuni kidogo |
| Lengo 15: Misha ya Nchi kavu | 15.1.1 Eneo la msitu kama sehemu ya jumla ya ardhi<br>15.2.1 Maendeleo kuelekea usimamizi endelevu wa msitu | Mradi utapunguza matumizi ya kuni kwa sababu ya ufanisi mkubwa wa ICS, hivyo kupunguza ukataji miti na kulinda misitu |

## 5. Taarifa za mawasiliano kwa maelezo ya kiufundi na Habari za Mradi

Iceberg: Mr. Ji BAO

Barua pepe: baoji@icebergchina.com

Mratibu wa Mradi: Mr Simkwai

Barua pepe: privatussimon5@gmail.com

Phone: 0693267720/0715930401

Tafadhari jisikie huru kuwasiliana nasi kwa maswali yoyote